Namba ya Mtahiniwa: ..............................

# BARAZA LA WAKUU WA SHULE ZA KIISLAMU TANZANIA

# MTIHANI WA UTAMILIFU WA SHULE ZA KIISLAMU

## KIDATO CHA PILI

**015** **ELIMU YA DINI YA KIISLAMU**

**MUDA: Saa 2:30** **Jumatano, 05 Agosti 2026 mchana**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali kumi (10).
2. Jibu maswali yote.
3. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu yenye wino wa bluu au mweusi.
4. Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizopewa.
5. Vifaa vya mawasiliano na vitu visivyoruhusiwa havitakiwi katika chumba cha mtihani.
6. Andika namba yako ya mtihani katika kila ukurasa sehemu ya juu upande wa kulia.

| KWA MATUMIZI YA MTAHINI TU | | |
|---|---|---|
| **NAMBA YA SWALI** | **ALAMA** | **SAINI YA MTAHINI** |
| 1 | | |
| 2 | | |
| 3 | | |
| 4 | | |
| 5 | | |
| 6 | | |
| 7 | | |
| 8 | | |
| 9 | | |
| 10 | | |
| **JUMLA** | | |
| **SAINI YA MKAGUZI** | | |

Shulelibrary.com

Namba ya Mtahiniwa: .............................

**SEHEMU A (Alama 15)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

1. Katika kipengele (i) – (x), chagua jibu sahihi kisha andika herufi yake katika jedwali ulilopewa.

(i) *"Tuongoze katika njia iliyonyooka, sio ya waliokasirikiwa wala waliopotea."* (Suratul-Faatiha: 7. Kwa mujibu wa aya hii, ni akina nani waliopotea?

A. Wayahudi
B. Wanaswara
C. Wamajusi
D. Wapagani

(ii) Katika khutba ya Ijumaa, Khatibu alifafanua vitabu sita mashuhuri vya Hadith sahihi za Mtume (S.A.W) na waandishi wake. Kwa taaluma ya Hadith uliyonayo, ni vitabu gani miongoni mwa alivyoviwasilisha?

A. Sahihi Muslim na Bukhari
B. Al-qatadayah na Al- Muwatwau
C. Sunanu Ahman na Al-Muwatwau
D. Sahihi Sunnah na Bukhar

(iii) Rafiki yako, Mabo anasema kuwa suala la kuamini uwepo wa Allah (S.W) ni "ububusa". Wewe kama mtaalamu wa Elimu ya Dini ya Kiislamu, utampa hoja gani kukanusha dai lake?

A. Msisitizo wa kuswali swala tano katika Uislamu
B. Msisitizo wa kuwafanyia wema wazazi wawili
C. Msisitizo wa elimu zote katika Uislamu
D. Msisitizo wa kufanya ibada kwa ujumla katika Uislamu

(iv) Bibi Sozi ni mtalaamu wa mambo ya Uchumi wa Kiislamu na siasa. Bibi huyu ni mjuzi wa fani gani ya Elimu ya Dini ya Kiislamu?

A. Fiqh Muamalat
B. Fiqh ya Kisiasa
C. Fiqh Ibaadat
D. Fiqh Islamiyyah

(v) Wanafunzi wa kidato cha pili wamesahau nguzo za Daáwa. Wewe kama kijana unayefanya kazi ya kulingania, wakumbushe wenzako nguzo hizo.

A. Qurán, da'ia na hadhira
B. Da'i, hadhira na ujumbe
C. Qurán, Sunnah na Ijtihad
D. Ujumbe, hadhira na Sunnah

Shulelibrary.com

(vi) Ndugu yako amekerwa na mkewe, akapatwa na hasira na kufanya kosa la kumfananisha mkewe na mama yake mzazi. Je, Ni jambo gani ndugu huyu anapaswa afanye ili asameheke kwa kosa hilo?

A. Kumlipa fidia mke wake
B. Kulisha masikini mmoja kila siku
C. Kuwaacha huru watumwa wawili
D. Kufunga miezi miwili mfululizo

(vii) Swala haiwezi kukamilika bila ya kutekeleza masharti yake kikamilifu. Bainisha jozi inayoelekeza masharti hayo kwa usahihi.

A. Kuchunga wakati na khushui
B. Twahara na khushui
C. Twahara na stara
D. Stara na khushui

(viii) Wakati wa kusoma Qur'an Kheri alisikika akiichanganya herufi katika herufi nyingine na kutamka kama herufi moja yenye mkazo (Shaddah). Ni hukumu gani ya Taj-wiid inayopatikana kwa usomaji huo?

A. Id-ghaam
B. Ikh-faau
C. Iq-laab
D. Idh-haar

(ix) Mwandishi mmoja aliandika kwenye kitabu chake kuwa Dini ni jambo la kupingwa ili kuinusuru jamii kutokana na unyonyaji na ukandamizaji unaosababishwa na uwepo wa Dini. Dai hili si sahihi kwa mtazamo upi?

A. Ukafiri
B. Upagani
C. Utawa
D. Uislamu

(x) Nabii Adam (A.S) katika Maisha yake yote alikuwa anaandaliwa kuwa Khalifa. Jambo gani linaloonesha usahihi wa hili?

A. Kuwashinda Malaika kielimu
B. Kupewa elimu zote muhimu
C. Kuumbiwa kila kitu duniani
D. Kuishi peponi yeye na mkewe

**MAJIBU:**

| (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) | (vi) | (vii) | (viii) | (ix) | (x) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | |

Shulelibrary.com

2. Kwa kuzingatia fani ya Fiqh, oanisha sifa za maji zilizo katika orodha A na aina za maji zilizo katika orodha B, kisha andika herufi ya jibu sahihi katika jedwali ulilopewa.

| ORODHA A | | ORODHA B |
|---|---|---|
| (i) | Maji yaliyo katika asili yake kabla ya kuchanganywa na kitu chochote. | A. Maji masafi |
| (ii) | Maji yaliyojazwa katika pipa lenye ujazo wa lita 3000 | B. Maji ya Bahari |
| (iii) | Maji yaliyo na sifa zote za kufaa kujitwaharishia | C. Maji mut-laq |
| (iv) | Maji safi lakini yamenywewa na paka na kubakishwa | D. Maji machache |
| (v) | Maji yaliyojaa katika pipa kubwa lenye ujazo wa lita 200 | E. Maji mengi |
| | | F. Maji ya mto |
| | | G. Maji makombo |

**MAJIBU:**

| **ORODHA A** | (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) |
|---|---|---|---|---|---|
| **ORODHA B** | | | | | |

**SEHEMU B (Alama 70)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

3. Halima ameolewa, ana miezi sita katika ndoa yake na kumetokea kutokuelewana baina yake na mumewe na utafiti unaonesha chanzo ni Halima hajui wajibu wake kama mke. Muelimishe Halima mambo manne (4) anayowajibika kuyaishi ili kunusuru ndoa yake.

(i) ______________________________________________

______________________________________________

(ii) ______________________________________________

______________________________________________

(iii) ______________________________________________

______________________________________________

(iv) ______________________________________________

______________________________________________

4. Samadu aliuliza swali katika kundi la Waislamu, “Kwanini Qur’an yenu haikushushwa siku moja yote kwa Pamoja?” Wote walikosa jibu. Je, ingekuwa wewe ungetoa jibu gani? Toa sababu nne (4).

(i) ______________________________________________

______________________________________________

(ii) ______________________________________________

______________________________________________

(iii) ______________________________________________

______________________________________________

(iv) ______________________________________________

______________________________________________

Shulelibrary.com

5. Umeteuliwa kuwafikishia ujumbe wa Uislamu wanafunzi waliosilimu shuleni kwenu. Mambo gani matano ukiyazingatia, ujumbe huo utakuwa bora na wenye athari nzuri kwao?
(i) ______________________________________________
______________________________________________
(ii) ______________________________________________
______________________________________________
(iii) ______________________________________________
______________________________________________
(iv) ______________________________________________
______________________________________________
(v) ______________________________________________
______________________________________________

6. Mbinu alizokuwa amezitumia Nabii Ibrahim (A.S) katika kufikisha ujumbe wa Mwenyezi Mungu (S.W) kwa jamii yake ni mbinu bora kabisa ambazo hata leo tukizitumia tutapata mafanikio katika jukumu la kufikisha ujumbe wa Mwenyezi Mungu (S.W). Kutokana na mbinu hizo ni mafunzo gani matano (5) tunayapata katika jukumu la kufikisha dini ya Mwenyezi Mungu (S.W)?
(i) ______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
(ii) ______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
(iii) ______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
(iv) ______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
(v) ______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

Shulelibrary.com

7. Umealikwa shule Jirani kushiriki mdahalo wa kidini unaohusu suala la uwepo wa Allah (S.W). Makafiri wakatoa hoja nyingi zinazoonesha kutokuwepo kwake! Wewe kama Muislamu;
(a) Bainisha hoja mbili tu miongoni mwa walizozitoa makafiri hao.
(i) ______________________________________________
______________________________________________
(ii) ______________________________________________
______________________________________________
(b) Chambua udhaifu wa kila dai lililotajwa (a) kwa hoja moja moja.
(i) ______________________________________________
______________________________________________
(ii) ______________________________________________
______________________________________________

8. Miongoni mwa wanayojifunza Waislamu kutokana na Suratul-Faatiha ni kuanza kila jambo jema kwa Bismillah. Tathmini faida nne zinazoweza kupatikana kwa kuanza kwa utajo huo.

(i) ______________________________

______________________________

(ii) ______________________________

______________________________

(iii) ______________________________

______________________________

(iv) ______________________________

______________________________

9. Kutoka kwa Abuu Huraira (R.A) hakika Mtume (S.A.W) amesema: "Alama za mnafiki ni tatu; akizungumza husema uongo, akitoa ahadi hatimizi na akiaminiwa hufanya khiyana." (Bukhari na Muslim). Kutokana na Hadith hii;

(a) Bainisha maana ya;

(i) Kuchunga ahadi

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

(ii) Uaminifu

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

(b) Eleza kwa ufupi faida tatu za mtu kuwa mwaminifu katika jamii

(i) ______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

(ii) ______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

(iii) ______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

Shulelibrary.com

Namba ya Mtahiniwa: ..............................

**SEHEMU C (Alama 15)**

Jibu swali la **kumi (10)**

10. Darila ni binti anayewajibika kufunga Ramadhani lakini hafungi kwa madai kuwa anashinda na njaa bila ya faida yoyote. Wewe kama mjuzi wa Elimu ya Dini ya Kiislamu, tumia hoja nne kumuonesha binti huyu umuhimu wa ibada hiyo ili aondokane na dhana potofu aliyonayo.

Shulelibrary.com

Namba ya Mtahiniwa: ..............................

*Wabillah Tawfiiq*

Shulelibrary.com